

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**OFISI YA RAIS**  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO

Simu Na. 023 2440338  
FAX Na. 023 22440338



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
S.L.P. 59,  
**BAGAMOYO.**

**TAARIFA KWA UMMA NA VYOMBO VYA HABARI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo anawakaribisha Wananchi wote wa Bagamoyo na maeneo jirani, kwenye ziara maalumu ya Mhe. Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Bi. Samia Suluhu Hassan itakayofanyika siku ya Jumatano Tarehe 24 na 25 Oktoba, 2018.

Mhe. Makamu wa Rais, Bi. Samia Suluhu Hassan siku ya Tarehe 24 Oktoba, 2018, kuanzia saa 9:30 Alasiri atatembelea Shamba la Kuku wazazi lililopo Kata ya Yombo na kukagua shughuli za ufugaji wa Kuku kisha ataelekea Hoteli ya Oceanic Bay iliyopo Bagamoyo Mjini ambako atapokea taarifa ya Mkoa na Wilaya zote za Mkoa wa Pwani.

Siku ya Tarehe 25 Oktoba, 2018 Mhe Makamu wa Rais Bi. Samia Suluhu Hassan, kuanzia saa 3:00 Asubuhi, atatembelea eneo la Mbegani ambako kunatarajiwa kujengwa bandari mpya ya Bagamoyo, atatembelea na kuzindua kiwanda cha kutengeneza mabati cha African Dragon kilichopo Zinga, pia atatembelea na kukagua ujenzi wa tanki la maji la DAWASCO lililopo Kata ya Magomeni, kisha atazungumza na Wananchi katika Mkutano wa hadhara kwenye Viwanja vya Shule ya Msingi Majengo.

Wananchi wote mnakaribishwa.

Imetolewa na;

Kitengo cha Teknolojia, Habari, Mawasiliano na Uhusiano

Halmashauri ya Wilaya

**BAGAMOYO**

22/10/2018

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
BAGAMOYO**